

**Tasnifu: Ufundi (wa) Magari, Mfano wa
Ukuzaji wa Istilahi za Kiswahili
Mwandishi: Ridder H. Samson (1988)**

Mpitiaji: Seleman S. Sewangi

Utangulizi

Tasnifu inayopitiwa hapa, iliandikwa kwa ajili ya Shahada ya Pili (M.A.) katika Isimu na Lugha za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Leiden, Uholanzi. Tasnifu hiyo ambayo imeandikwa kwa Kiswahili, ni matokeo ya utafiti wa mwandishi hapa Tanzania katika kipindi cha 1983 hadi 1984. Kwenye Utafiti huo, alisaidiwa na watu mbalimbali akiwemo Profesa Batibo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kulingana na mwandishi, utafiti wake, ulichochoewa na kutokuwepo kwa uchunguzi mkubwa uliofanyika katika kufahamu matokeo ya kazi za Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) kuhusu kazi yake ya kusanifu lugha (uk. 1). Hivyo, lengo lake lilikuwa ni kutoa picha ya uhusiano baina ya ukuzaji huru wa istilahi na ukuzaji unaoongozwa kwa kulinganisha matumizi huru katika mahala pa kazi au maandishi na Istilahi Sanifu za BAKITA.

Lengo la mapitio haya ni: kwanza, kutoa muhtasari wa tasnifu hiyo ili kumwezesha yule ambaye hajaisoma kupata picha halisi ya yale yaliyomo kwenye tasnifu hiyo; pili kuonyesha umuhimu wa kazi hiyo katika mazingira ya sasa ya Kiswahili hasa katika uwanja wa istilahi za ufundi magari; mwisho kufanya tahakiki katika baadhi ya vipengele vya tasnifu hiyo.

Muhtasari

Sura ya Kwanza

Sura hii inahusu nadharia juu ya ukuzaji na usanifishaji wa istilahi. Imegawanyika katika sehemu nne.

Sehemu ya kwanza inahusu tabia ya jumla ya lugha; kwamba hubadilika katika viwango vyake vyote; sauti, maneno, kiimbo, sentensi na msamiati. Msingi

wa mabadiliko ya msamiati wa lugha ni mazingira. "Mazingira yakigeuka msamiati hugeuka. Maneno mapya huzuka wasemaji wanapoanza kuzungumza mambo mapya" (uk. 6). Mabadiliko haya ndiyo msingi wa ukuzaji istilahi. Mabadiliko makubwa na ya haraka katika mazingira ya Kiswahili ndicho kichocheo kikubwa cha mahitaji ya istilahi za fani mbalimbali.

Sehemu ya pili inatoa fasili ya istilahi. Mwandishi anasema, "maana ya istilahi ni neno ambalo limeunganishwa na dhana za fani maalumu" (uk. 10). Isipokuwa tu kwa maneno yaigayo sauti au kitu kilichotajwa, hakuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya dhana na istilahi yake. Mambo makubwa mawili huchochea ukuzaji wa istilahi: kupanuka kwa haja ya mawasiliano na kuendelea kwa teknolojia. Ukuzaji wa istilahi upo wa aina mbili, ukuzaji huria ambao hufanywa na watumiaji mara tu haja ya istilahi mpya inapozuka, na ukuzaji unaoongozwa, ambao hufuata sera ya serikali na kushughulikiwa na vyombo vya lugha.

Undaji wa Istilahi za Kiswahili, hufanywa kwa kutumia njia sita: maneno pacha, minyambuliko, kuyapa maneno matumizi mapya, kubuni, kukopa na kutafsiri dhana za kigeni (uk. 13). Kulingana na Ohly (1976:27), yapo makundi matatu yanayoshughulikia ukuzaji wa Istilahi. "Tanga School" hutumia mashina ya Kiswahili chenyewe kama msingi wa ukuzaji istilahi, mfano, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI); "Zanzibar School," hutegemea ukopaji kama msingi wa ukuzaji istilahi; na "kundi la mseto" ambalo hutumia njia zote mbili (uk.15).

Sehemu ya tatu inahusu usanifishaji kwa jumla. Maana ya Usanifishaji ni kukifanya kitu fulani kilingane na hadhi fulani. Hadhi hiyo ni kipimo cha ulinganishi wa thamani au tabia. Usanifishaji unahusu pia dhana (uk. 18). Tofauti katika matumizi ya lugha kwenye jamii pana huleta haja ya Usanifishaji wa lugha. Usanifishaji wa lugha ni kazi ya kuondoa hitilafu zozote zile ambazo huwakwaza watumiaji katika kuelewana.

Usanifishaji wa istilahi, umejadiliwa katika sehemu ya nne. Usanifishaji huu husababishwa na haja ya kuweko kwa mawasiliano yaliyo wazi katika fani za ufundi, uchumi na sayansi. Kulingana na Gilinski (1982), iko misingi minne ya usanifishaji wa istilahi; usanifishaji huu utangulie ule wa kiteknolojia. Lengo la usanifishaji huu ni ufanisi wa lugha. Matumizi yaliyoko yasibadilishwe bila sababu ya maana; usanifishaji wa istilahi ufanywe na kikundi cha wataalam (jopo, uk. 27). Usanifishaji wa Istilahi lazima ufanyike kulingana na misingi ya kimataifa iliyowekwa na ISO.

Kabla ya BAKITA, istilahi za Kiswahili zilisanifishwa na Inter-Territorial Language Committee; chombo kilichoundwa na wakoloni. Njia zilizotumiwa na chombo hicho katika kukuza istilahi zilikuwa ni kuchukua neno la kigeni bila mabadiliko yoyote, kutohoa na kupanua maana ya neno (uk. 31). Hata hivyo baadhi ya istilahi zilizoundwa na chombo hiki hazikukubalika kwa watumiaji.

Sura ya Pili

Asili na mazingira ya matumizi ya data vinafafanuliwa katika sehemu ya kwanza. Asili hizo zikiwa zimeambatanishwa na jumla ya istilahi zao ni; BAKITA (186), GEREJI (129), KARAKANA (132), CHUO (80), NKONDOKAYA 1 (202), NKONDOKAYA 2 (71), SCANIA (228) na WIZARA (116).

Katika jumla ya istilahi za BAKITA istilahi 130 zilitoka Kilombero kwa Afisa Mafunzo ambaye aliomba BAKITA izisanifishe ili aweze kuzitumia katika kazi yake aliyokuwa akiifanya. Istilahi hizo zote zilihusu injini za petroli tu, hakuna istilahi hata moja itajayo sehemu maalum kutoka katika injini za dizeli (uk. 39).

Istilahi za GEREJI zimetoka K.J. Motors ambayo iko

Dar es Salaam. Istilahi hizi zinahusiana na injini zote za petroli na za dizeli. Kwa vile maelezo ya fundi aliyehojiwa yalikuwa ya jumla istilahi nyingi hazitaji vipuri maalum vya gari (uk. 40).

Istilahi za KARAKANA, zilikusanywa kutokana na maelezo ya fundi.

Istilahi za CHUO zilikusanywa toka darasani wakati wa kipindi cha somo juu ya "Kazi za Vali."

Istilahi za NKONDOKAYA 1 na 2 zimetoka kwenye vitabu vya: *Matatizo ya gari na marekebisho yake* (1983) na *Injini za dizeli* (1983), vitabu vilivyoandikwa na J.R. Nkondokaya.

Istilahi za SCANIA zimetoka kwenye tafsiri ya kijitabu kitiwacho: *Operators manual*. Kijitabu hiki kinaeleza juu ya Scania LB/81/86/111; uendeshaji pamoja na utunzaji wa Scania (uk. 47).

Istilahi za WIZARA, zimetoka kwenye mtihani wa Taifa wa Ufundi (Nadharia daraja la III), 1982.

Sehemu ya pili inaainisha vigezo vya upambanuzi wa data. Vigezo vilivyoainishwa ni: Mkopo, Tafsiri muazimo, Mchanganyiko na Nyingine (uk. 55-58). Vigezo vingine ni "Pekee" na Ambatano. Chini ya "Pekee" zimewekwa istilahi zote zenye shina moja, na chini ya "Ambatano" istilahi zenye zaidi ya shina moja. Pia ametoa vigezo vya majina yanayoishia na jina litendalo ambalo huishia na -a, -i au -aji.

Upambanuzi wa istilahi kulingana na vigezo vya upambanuzi umefanywa katika sehemu ya tatu. Vielelezo vya duara na majedwali vimetumika katika kuonyesha upambanuzi huo.

Sura ya Tatu

Uchambuzi wa data na matokeo ya uchambuzi vinatolewa hapa. Lengo la uchambuzi ni kulinganisha

istilahi za ukuzaji huru na za ukuzaji unaoongozwa. Asili za data zimewekwa katika makundi matatu: kundi la istilahi zilizotokana na usanifishaji rasmi kutoka juu-BAKITA, kundi la istilahi zilizotokana na usanifishaji toka juu ambao unatekelezwa kwa vitendo (NKONDOKAYA 1 na 2, SCANIA, na WIZARA) na kundi la istilahi zilizotokana na utiifu na utekelezaji wa wasemaji (GEREJI, KARAKANA na CHUO, uk. 81).

Uchambuzi wa data unafanywa kwa kutumia vielelezo vya majedwali na vya duara. Kutokana na uchambuzi huo, mahitimisho yafuatayo yanatolewa;

BAKITA ina istilahi pekee chache ikilinganishwa na asili nyingine. Hii inaonyesha kuwa istilahi za BAKITA hutaja mambo au vitu maalum zaidi kuliko za asili nyingine.

Istilahi nyingi za BAKITA zinataja vitu au mambo yasiyotajwa na asili nyingine.

Istilahi za BAKITA hazitoshi kwa watumiaji wa lugha kuelezea gari na kazi zake.

Istilahi za BAKITA ni maalum sana; istilahi za asili nyingine ziko katika kiwango cha "mahala pa kazi" na zile za BAKITA ziko katika kiwango cha "Istilahi."

Kiasi cha istilahi za mkopo katika BAKITA ni kidogo kuliko asili nyingine zote. Kiasi hicho ni asilimia 18 tu ya istilahi zote za BAKITA.

Kiasi kikubwa cha istilahi za BAKITA kinatokana na kutafsiri maneno ya Kiingereza. Mtindo huu unavuta zaidi wale wanaojua Kiingereza kwani uwazi wa istilahi iliyotafsiriwa unategemea ujuzi wa msemaji wa Kiingereza.

Ipo mitindo inayotumiwa na BAKITA katika kuunda istilahi ambayo haitumiwi na asili nyingine; kudondoshwa kwa 'a' ya uhusiano, kuundwa kwa jina litendalo, kuunda maneno pacha, na tafsiri muazimo. Mitindo inayopendelewa na asili nyingine ni: Uthoaji

wa istilahi za Kiingereza, minyambuliko, matumizi ya '-a' ya uhusiano, na matumizi ya vitenzijina.

Istilahi nyingi za asili nyingine hazina tafsiri sanifu ya BAKITA.

Tofauti zilizojidhihirisha baina ya istilahi za BAKITA na zile za asili nyingine zinaonyesha kuwa athari za BAKITA katika Taasisi hizo juu ya matumizi ya lugha ya kiufundi ni ndogo sana. Hali hii inaweza kuwa imetokana na: istilahi kuwa mbali na watumiaji, uenezaji wa istilahi kutotosha, istilahi kutotosheleza, istilahi kutoeleweka, na tofauti za mitindo ya kiisimu baina ya BAKITA na watumiaji wengine.

Mwisho mwandishi anaeleza hali halisi ilivyo katika usanifishaji wa Kiswahili. Anadai kuwa kanuni zinazotumika katika kusanifisha Kiswahili, si wazi wala imara. Kwa mfano upo utatanishi juu ya kutumia au kutotumia '-a' ya uhusiano katika kuunda maeno pacha na tofauti kati ya lugha ya karakana na istilahi. Kwa upande wa maandishi pia kuna utatanishi; je, iandikwe "mtaimbokombo au mtaimbo kombo"?

Anamaliza kwa kusesitiza kuwa, usanifishaji wa istilahi, ni lazima utazamwe katika mapana ya uhusiano wa lugha na jamii na pili, Kiingereza kipewe umuhimu wa kwanza kama lugha kopeshi katika ukuzaji wa istilahi za ufundi magari.

Umuhimu wake

Uchambuzi mfupi wa mazingira ya istilahi za ufundi magari na historia yake katika Kiswahili utasaidia kuonyesha umuhimu wa kazi hii katika Kiswahili. Fani ya ufundi magari haina historia ndefu katika mazingira ya Kiswahili. Gereji ya kwanza katika Tanzania ilianzishwa mjini Dar es Salaam mwaka 1923 (Njovu, katika Samson 1988:77). Kutokana na kutokuwako kabisa kwa istilahi za fani hii katika Kiswahili, istilahi zilizotumika mwanzoni kabisa, na hata baadaye Waswahili walipoanza kujishughulisha na fani hii, zilitokana na Kiingereza. Hali hii imeendelea hadi sasa kwani, hadi kufikia mwaka

1987, istilahi sanifu za fani hii zilikuwa hazizidi 200 (Samson 1988:39).

Hata hivyo, juhudi mbalimbali zimekuwa zikifanywa na vyombo mbalimbali vya ukuzaji wa Kiswahili katika kuongeza istilahi za fani hii; mwaka 1986, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ilitoa orodha yenye jumla ya istilahi 1150 za fani hii, hasa upande wa matrekta aina ya Valmeti. Vyombo vya Ukuzaji Kiswahili hufanya kazi hii kulingana na kanuni za BAKITA ambazo zimeweka kipaumbele katika kukitumia Kiswahili chenyewe kama msingi wa kupatia istilahi. Kulingana na kanuni hizo (Kakulu 1982:15) matumizi ya lugha za kigeni (ukopaji) yamepewa nafasi ya mwisho katika kutoa istilahi.

Kwa watumiaji, kukosekana kwa istilahi za Kiswahili za fani hii, kumewafanya waendeleo kutumia Kiingereza kama chanzo kikuu cha kupatia istilahi kila haja inapozuka. Hivyo kwa upande mmoja, vipo vyombo vya ukuzaji Kiswahili vinavyoongozwa na BAKITA ambavyo vinatumia Kiswahili kama chanzo kikuu. Na upande mwingine, wako watumiaji ambao wanalazimishwa na kutokuweko kwa istilahi za Kiswahili kutumia Kiingereza kama chanzo kikuu cha kupatia istilahi kila haja inapozuka.

Hali hii inaweza kusababisha mvutano, baina ya vyombo vya ukuzaji lugha na watumiaji wa istilahi za fani hii.

Ili kuondoa hali hiyo, ambayo inaweza kuwa kikwazo katika ukuzaji wa istilahi, ni lazima ufanyike uchunguzi ambao utawahusisha watumiaji na vyombo vya ukuzaji. Akizungumzia umuhimu wa uchunguzi kama huo, MacWilliam (1986) anasema:

"Taaluma ya istilahi ni ya kimatumizi, hivyo ipo haja kubwa kwa wataalam wanaohusika na ukuzaji wa lugha, upande wa istilahi, kuwaendea watumiaji badala ya kukaa maofisini mwao wakisanifu istilahi nzuri ambazo hazitakubalika kwa mafundi magari,

wajenzi wa mabarabara, mafundi umeme, na mafundi bomba" (Tafsiri yangu).

Ni dhahiri kwamba, kama tofauti baina ya wakupaji lugha na watumiaji hazitaondolewa, kuna hatari ya istilahi za fani hii zinazoundwa na vyombo vya kukuza Kiswahili kutotumiwa na mafundi magari. Kwa mfano, mwandishi wa Tasnifu hii, anaeleza kuwa, kwa jumla istilahi za BAKITA, isipokuwa tu zile za mikopo hazipendelewi na watumiaji (taz. uk. 106 wa tasnifu).

Kuweko kwa istilahi sanifu chache za fani hii, kunaonyesha kuwa, hata kama watumiaji wangekuwa tayari kutumia istilahi za BAKITA, bado wangekwama kwani hazitoshelezi mahitaji yao. Swali ambalo bado lingeendelea kuwepo ni: je, hilo pengo kwa watumiaji litazibwa vipi, hasa ikizingatiwa kwamba uundaji wa istilahi sanifu huchukua muda mrefu. Ili kujibu swali hili, Ohly (katika Samson 1988) anasema kuwa ni vyema kwenda kwa watumiaji ili kuona wanachofanya. Tasnifu hii, ni kazi mojawapo ambayo inatupeleka hadi kwa watumiaji na kutuonyesha uhusiano baina ya chombo kikuu cha usimamizi wa ukuzaji wa Kiswahili (BAKITA) na watumiaji lugha katika mazingira yao halisi. Taarifa zinazotokana na utafiti huo, zitatumwa na wakuza lugha katika kufanya tathmini juu ya ukubalifu wa kazi zao kwa watumiaji waliokusudiwa.

Matokeo ya tathmini kama hiyo, yatasaidia katika kuchagua mbinu ya ukuzaji istilahi za fani hii ambayo itafanikisha kuondoa mvutano ulioko.

Kazi hii pia inatoa mchango mkubwa katika nadharia ya istilahi na jinsi nadharia hiyo inavyoweza kutumika kukuza istilahi za Kiswahili. Mchango huo, utasaidia katika madarasa ya wanafunzi wa Isimu upande wa Istilahi.

UPUNGUFU

Ukuzaji wa Istilahi

Katika kipengele hiki, zimetajwa njia kuu sita za

kupatia Istilahi (uk. 15). Hata hivyo haikuelezwa kama uainishaji wa njia hizi umetokana na mwongozo gani. Misingi ya uainishaji pia haikuelezwa. Kulingana na BAKITA, ipo misingi mikuu miwili ambayo ni: kutumia Kiswahili chenyewe na lahaja zake na kutumia lugha nyingine, yaani kukopa (Kakulu 3, 1982:15). Hivyo, mwandishi angepaswa aanze kwa kubainisha misingi hii, kisha aorodheshe njia zake chini ya kila msingi. Jedwali lifuatalo linaonyesha mfano wa uainishaji huo:

Misingi mikuu miwili ya kupatia istilahi za Kiswahili kutumia

Kiswahili chenyewe

**Njia zinazotumika:
zinazotumika:**

- Kutumia visawe
- kupanua maana ya neno

- kuunganisha maneno

- kunyambulisha

Kukopa

Njia

- kutohoa
- kutafsiri
- tafsiri huru

- tafsiri muazimo
- kuasilisha

Kukosekana kwa misingi ya uainishaji wa njia za kuundia istilahi, kunasababisha uainishaji unaotatanisha wenye mwingiliano. Kwa mfano, mwandishi anadai kuwa istilahi "hataza" ambayo imetokana na maneno "hati ya kukataza" imetokana na njia ya kubuni (uk. 15). Lakini istilahi hiyo imetokana na njia ya kutumia mifito.

Maneno "dingi" na "dezo" yameelezwa kuwa ni mapya na asili yake haijulikani (uk. 15). Maneno haya hayana hadhi ya istilahi bali ni simo ambazo huzuka kwenye jamii ndogondogo za lugha na mara nyingi hutoweka baada ya muda.

Katika kupambanua lugha zilizoendelea na zinazoendelea, mwandishi ametumia dai la Ferguson (1968)

kuwa lugha iliyoendelea ina kiasi cha istilahi zinazoiwezesha kufanya kazi zote za Taifa. Kisha anaeleza kuwa kulingana na Ohly (1976) hadi kufikia mwaka 1976, Kiswahili kilikuwa na istilahi 5,000 na kilihitaji jumla ya istilahi 25,000 au zaidi ili kifikie kiwango cha lugha iliyoendelea (uk. 14). Kwa maneno mengine, mwandishi anakubaliana na Ohly kuwa Kiswahili kikiwa na jumla ya istilahi 30,000 kitakuwa kimeendelea. Kukubali hoja hii ni kukubali kuwa maendeleo ya lugha yana ukomo. Pia ni kutokubali ukweli kuwa maisha ya binadamu na mazingira yake vimegawanyika katika fani nyingi ambazo pia zimegawanyika katika vikoa vingi. Felber (1980) anatudokezea kuwa fani ya uhandishi umeme peke yake ina dhana milioni nne. Iweje tujidanganye kuwa Kiswahili kitakuwa na uwezo wa kukidhi mahitaji yote ya taifa kitakapofikisha istilahi 30,000 tu! Kigezo cha kutumia idadi kadhaa ya istilahi za lugha fulani katika kupima maendeleo ya lugha sio imara kwani idadi ya istilahi katika lugha hulazimika kubadilika mara tu haja mpya inapozuka. Haja mpya ya istilahi yaweza kusababishwa na ugunduzi wa mambo mapya au mwingiliano wa mawasiliano baina ya jamii mbili tofauti.

Kwa kutumia dai la Ohly (1976) mwandishi ametaja makundi matatu yanayoshughulika na ukuzaji wa istilahi za Kiswahili. Msingi wa uainisho huo ni njia inayotumiwa na kila kundi katika kukuza istilahi za Kiswahili (uk. 15). Hata hivyo, baada ya kuyataja makundi hayo, hayaonyeshi popote katika kazi yake kama kweli makundi hayo yako au la. Kutokuonyesha huko kunamwacha msomaji katika hali ya utatanishi. Kwanza hataelewa kama hayo makundi yapo kweli, na pili atajiuliza sababu za kutajwa kwa makundi hayo na mwandishi kwani hayakutumika mahali pengine popote katika kazi hii.

Uteuzi wa Data

Vyanzo (asili) na sehemu za gari zilikutoka istilahi (data) zilizotumika katika kazi hii ni kama ifuatavyo:

CHANZO

SEHEMU YA GARI

1. BAKITA
Injini za petroli
(haikuelezwa kama ni
sehemu gani za injini)
2. GEREJI
Injini za petroli na
dizeli (sehemu za
injini hazikutajwa)
3. KARAKANA
Haikuelezwa
4. CHUO
Vali (Valve)
5. NKONDOKAYA 1 & 2
Sehemu mbalimbali za
gari zikiwemo injini za
dizeli
6. SCANIA
Zinahusu Scania
(LB/81/86/111).
Ni za jumla juu ya
uendeshaji na
utunzaji wake
7. WIZARA
Ufundi magari kwa jumla
(mitihani ya ufundi
uk. 37-48)

Ni dhahiri kuwa data ya mwandishi haitoki katika sehemu moja ya gari kwa vyanzo vyote. Hapa tunajiuliza, msingi wa uteuzi wa data hii ni upi? Bila shaka msingi huo ulikuwa ni "Ufundi magari". Hata hivyo "ufundi magari" ni fani pana ambayo si rahisi kwa mtafiti kuizamia yote kwa wakati mmoja. Msingi huo wa uteuzi wa data umesababisha matatizo katika ulinganishaji wa data kama itakavyoonekana baadaye.

Vigezo vya Upambanuzi wa Data:

Mwandishi ametaja vigezo vya upambanuzi (uk. 55-65) wakati akipambanua data yake. Hata hivyo, msingi wa uteuzi wa vigezo hivyo haukuelezwa. Uainishaji huo

ungeweza kufanywa chini ya misingi mikuu miwili; msingi wa njia iliyotumika kupatia istilahi na msingi wa umbo la istilahi. Kwa njia hii, uainishaji wa vigezo ungeweza kuwa kama huu ufuatao:

ISTILAHU ZILIZOTOKANA NA
NJIA YA:

- Kuchukua visawe
- Kupanua maana
- Kunyambulisha
- Kutumia mifito
- Kutohoa
- Kutafsiri
- Kuasilisha

ISTILAHU ZENYE UMBO
LA:

- Pekee
- ambatano N + a(uhusiano)+N
(mf. breki ya upepo)
T(jina)+N
(mf. Kitanua Breki)
N+T. (mf. mtaimbo laza)

Minyambuliko Kiambishi-
ngeli + shina
+O (kigawo).

Kiambishi-
ngeli + shina
+ ji
(uporaji)

Hivyo kutokana na uainishaji huu, istilahi "kigawo" na "mzunguko" ambazo zimeorodheshwa chini ya nyingine (uk. 58) zingekuwa chini ya minyambuliko yenye umbo la kiambishi-ngeli+shina+O. Pia istilahi zilizoorodheshwa chini ya kigezo cha "Jina Litendalo" zingekuwa chini ya minyambuliko. Kwa njia hii vigezo vya mwandishi vingekuwa na mapana ya kutosha kuchukua

data kubwa.

Kukosekana kwa msingi bayana wa uainishaji wa vigezo vya upambanuzi, kumesababisha kuingiliana kwa vigezo wakati wa upambanuzi wa data. Kigezo cha "mkopo" (uk. 68-76) kinatumika katika vielelezo vya duara na jedwali, wakati ambapo kama data inavyoonyesha, vielelezo vya jedwali vinaonyesha upambanuzi wa istilahi kulingana na maumbo, na vile vya duara vinaonyesha upambanuzi huohuo kulingana na njia zilizotumika kupatia istilahi. Matumizi ya kigezo hiki kwenye upambanuzi wa istilahi kulingana na umbo, yanakanganya.

Matokeo ya Uchambuzi

Kutokana na msingi dhaifu wa uteuzi wa data na vigezo vya upambanuzi, mahitimisho yanayotokana na uchambuzi wa data, yanatia wasiwasi. Baadhi ya mahitimisho hayo ni haya yafuatayo:

BAKITA ina istilahi PEKEE chache ikilinganishwa na asili nyingine kwa vile istilahi za BAKITA zinataja mambo maalum kuliko zile za asili nyingine (uk. 83). Sababu aliyotoa mwandishi ni kuwa, istilahi za BAKITA zinataja vitu maalum zaidi kuliko zile za asili nyingine. Ni kweli kuwa data ya BAKITA haina istilahi nyingi za PEKEE, lakini sababu iliyotolewa hapa si lazima iwe ya kweli. Uchache huo, unaweza kuwa unatokana na njia inayotumiwa sana na BAKITA ya kutafsiri katika kupata istilahi. Data ifuatayo itasaidia kutetea dai hili.

ISTILAHU YA KIINGEREZA

KISAWA CHA BAKITA

KISAWA CHA ASILI NYINGINE

1. brake shoe	kiatu cha breki	brekishuu
2. short circuit	mkato saketi	shoti
3. connecting rod	pau piston	konrodi
4. crank shaft	mtaimbo kombo	krenkishafti
5. cylinder head	mfuniko wa silinda	silindahedi
6. dynamo	mota ya umeme	dainamo

7. fly wheel	gurudumu tegemeo	flaiwili
8. gear box	sanduku la gia	gia boksi
9. mainshaft	mtaimbo mkuu	menshafti
10. lay shaft	mtaimbo laza	leinshafti

Asili: Samson R. 1988 (sura ya nne)

Data hii inaonyesha kuwa istilahi zote za BAKITA sio za PEKEE (sio za neno moja) na zile za asili nyingine zote ni za PEKEE. Hata hivyo, kitu kinachotajwa na istilahi za BAKITA ni kilekile kinachotajwa na istilahi za asili nyingine. Hivyo tofauti ya umbo la istilahi hapa haisababishwi na umaalumu wa kitajwa bali inatokana na njia iliyotumika kupatia istilahi. Hivyo mwandishi alipaswa kufanya uchunguzi zaidi kabla hajatoa sababu yake.

Katika hitimisho lake jingine anasema kuwa BAKITA ina istilahi chache ambazo zinataja mambo au vitu vilivyotajwa na asili nyingine kwa sababu istilahi nyingi za BAKITA zinataja vitu maalum (uk. 83). Sababu iliyotolewa hapa pia inaleta wasiwasi kwani kulingana na uteuzi wa data (kama ilivyokwisha onyeshwa) inawezekana kuwa uchache huo unatokana na tofauti za sehemu za gari zilikutoka istilahi. Ni wazi kwamba istilahi za BAKITA ambazo ni za injini za petroli tu, zitataja vitu tofauti na zile za Scania ambazo zinatokana na gari zima.

Hitimisho jingine ni kwamba istilahi za BAKITA hazitoshi kuelezea gari na kazi zake (uk. 84). Jambo hili halikuhitaji hata kufanyiwa ulinganisho wa data kwa kuwa ni wazi kuwa istilahi za BAKITA zilizotumiwa na mwandishi (za injini za petroli tu) hazitoshi kuelezea gari zima na matumizi yake.

Kimsingi matatizo haya yote yanasababishwa na ukosefu wa mipaka katika data ya mwandishi. Data ya BAKITA ambayo imetokana na injini za petroli tu imetazamwa na kufanyiwa ulinganishi kama data inayotokana na fani nzima ya ufundi magari. Ukosefu wa mipaka katika uteuzi wa data, unamfanya mwandishi

ajikute akitumia data finyu katika fani pana kiasi kwamba matokeo ya uchambuzi yanakuwa ya wasiwasi kama tulivyoonyesha hapo juu.

Fani ya ufundi magari kama zilivyo fani nyingine ni pana sana. Hivyo kabla ya kuanza utafiti katika fani hii, mtafiti hana budi kujiwekea mipaka ya utafiti wake kwani sio rahisi kujumuisha vipengele vyote vya fani hii kwa wakati mmoja. Mtafiti wa kazi hii, hakuzingatia jambo hilo hivyo alijikuta akiukabili uwanja mzima wa ufundi magari kwa wakati mmoja. Bila shaka huu ndio uliokuwa mwanzo wa makosa yake katika uteuzi wa data. Njia bora ambayo angeweza kutumia ingekuwa ni kuchagua kipengele kidogo ndani ya fani ya ufundi magari, mfano, kipengele cha istilahi za injini za petroli. Na zaidi ya hapo angeweza akajibana zaidi kwa kuchagua kisehemu tu cha kipengele hiki kwa mfano: "Istilahi za Vali". Kisha utafiti wake ungeshughulikia data iliyotokana na kipengele alichochagua tu. Kufanya hivyo kungemwezesha kuwa na ulinganishi wenye mahitimisho imara kwani data yake ingekuwa na uhusiano mkubwa.

HITIMISHO

Makala haya hayakupitia kila kitu katika tasnifu hiyo. Muhtasari na uhakiki mfupi uliotolewa vimeonyesha machache tu katika yale yote yaliyomo. Hata hivyo, ni mategemeo yangu kuwa makala haya yatachochea hamu ya kuisoma tasnifu hiyo ili, kwanza, kupata yale yote yaliyomo ndani yake, na pili kulinganisha haya yaliyotolewa kwenye makala hii na yale yaliyomo ndani ya tasnifu hiyo.

MAREJEO

- Felber, H. 1980 "International Standardization of Terminology; Theoretical and Methodological Aspects." in *International Journal of Sociology of Language*, Vol. 23 uk.

- Irira, S. 1989 "Ukuzaji wa Istilahi". Makala isiyochapishwa iliyotolewa katika semina za BAKITA.
- Kakulu 1982 No. 3: Kamati ya Kusanifu Lugha, BAKITA.
- MacWilliam, A. 1986 "Report on Consultancy Project for Valmet Corporation 1986" (haijachapishwa). TUKI.
- Mwansoko, H.J. 1989 "The Principles, Methods and Procedures of Swahili Terminology Development in Tanzania; A Reexamination of Basic Issues" in *Journal of Asian and African Studies*, No. 38: uk. 161-176.
- Sansom, R.H. 1988 *Ufundi (wa) Magari: Mfano wa ukuzaji wa Istilahi za Kiswahili muhimu Tanzania. Matumizi na Usanifishaji wake. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Leiden Uholanzi.*